JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za simu:
Mkuu wa shule: 0655-972372/0782-972370
Makamu Mkuu wa Shule: 0762-932965
Patron : 0712056002

SHULE YA SEKONDARI KIGWE,
S.L.P 656,
DODOMA.
...../……../2022

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi

……..

……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI KIGWE HALMASHAURI YA WILAYA YA BAHI MKOA WA DODOMA - MWAKA 2022/23

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule ya Sekondari Kigwe mwaka 2022/23 tahasusi ya …… shule hii ni ya kutwa(day) kwa wanafunzi wa kidato cha I hadi cha IV, na kulala (Boarding) kwa wanafunzi wa kidato cha 5 na 6 wavulana.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule yetu ipo katika Wilaya ya Bahi, Kata ya Kigwe kilometa 35 Magharibi ya mji wa Dodoma. Utaweza kufika hapa kwa mabasi/daladala yajayo Kigwe ambayo kwa Dodoma mjini yanapatikana stendi mpya ya Mabasi yaendayo Bahi. Au kwa wanaokuja kwa gari moshi yaani treni watapaswa kushuka kituo cha gari moshi Kigwe.

Mwanafunzi ajapo shuleni aje na mahitaji yote na fomu husika zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu na kurudishwa mara ufikapo shuleni.

VIAMBATANISHO NI:

(i) Fomu ya kupima afya yake (FORM FOR MEDICAL EXAMINATION) ambayo itajazwa na daktari wa hospitali ya Serikali
(ii) Fomu ya habari za mwanafunzi ijazwe na Mzazi/Mlezi na isainiwe na mwanafunzi na Mzazi/Mlezi

KARIBU SANA



MWASITI B. MSOKOLA
MKUU WA SHULE



2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

(a) Shati 2 nyeupe za tetroni za mikono mirefu

(b) Suruali 2 za rangi ya Khaki ziwe na pindo (turn up)

(c) Viatu vya ngozi(vyenye kamba) jozi moja nyeusi vyenye visigino vifupi na viwe vya kubrashi na raba jozi moja zenye rangi moja kwa ajili ya michezo

(d) Soksi jozi 2 zenye rangi nyeupe

(e) Sweta la rangi ya kijani kibichi (dark green)

(f) Nguo za michezo (track na kaptura kwa ajili ya michezo)

- HGL – track rangi ya **KIJANI**
- HGK - track rangi **NYEKUNDU**

(g) Suruali nyeusi mbili (02) na t-shirt rangi ya kijivu mbili (02) hizi zinavaliwa baada ya masomo

(h) T-shirt nyekundu (hizi zitapatikana shuleni kwa bei ya Tshs. 10,000/=)

MUHIMU: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA MAVAZI TOFAUTI NA YALIYOELEKEZWA KWENYE FOMU HII.

3. ADA NA MICHANGO YA SHULE

(a) Ada ya shule ni Tshs. 70,000/= kwa mwaka au Tshs. 35,000/= kwa muhula

(b) Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila mwanfunzi ni:-

i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani

ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho

iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma

iv) Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.

v) Shilingi 10,000/= (kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya)

vi) Fedha ya tahadhari Tshs. 5,000/= (haitarejeshwa)

NB: Jumla ya ada na michango yote ni shilingi 156,000/=

ZINGATIA

Malipo yote ya ada na michango yalipwe kupitia Benki ya **NMB** Jina la A/C ni **Kigwe Sekondari A/C. No: 51701100037** jina la anayelipa liwe la mwanafunzi na si Mzazi / Mlezi. Mwanafunzi awasilishe **Pay-in-slip** ya Benki afikapo shuleni.

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

a) Ream moja ya karatasi (kwa mwaka)
b) Godoro la 2½
c) Mashuka 2 rangi ya light blue
d) Blanket 1
e) Chandarua 1 (square)
f) Mto 1
g) Taulo 1
h) Vyombo vya chakula (Sahani, kijiko, bakuli, kikombe)
i) Ndoo ya maji ya lita 10
j) Sanduku la bati (trunker) lenye kufuli kwa ajili ya kuhifadhi vifaa binafsi vya mwanafunzi.
k) Picha moja (1) ya Mzazi/mlezi na picha mbili (2) za mwanafunzi (Passport size)
l) Taa ndogo inayotumia umeme wa jua (solar) kwaajili ya dharura ya kukatika kwa umeme
m) Faili moja dogo kwaajili ya kuhifadhia kumbukumbu za kitaaluma
n) viifaa vya usafi - jembe lenye mpini, fyekeo, ufagio,dawa ya kufanyia usafi chooni (ARO),

(d) Vifaa vya darasani:-

- Daftari 9 aina ya Counter books (Quire 4) , Kalamu na penseli, Mathematical set na calculator (fx-991)

(e)Mambo mengine yakuzingatia

- Aje na nakala kivuli ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (result slip)
- Aje na fedha (pocket money) kwaajili ya matumizi yake binafsi

- **VITABU**

i) HISTORY

- Mastering history paper two/one
- Saleh Yassin, essential in advanced level history paper two/one

ii) KISWAHILI

- Tahakiki ya Kiswahili – kidato cha V na VI
- Kamusi ya Kiswahili sanifu
- Nadharia ya lugha Kiswahili I- kidato cha V na VI
- Nadharia ya fasihi Kiswahili II – kidato cha V na VI

iii) GEOGRAPHY

- Practical geography by Pritchard
- Secondary school atlas by MC MILLAN AIDAN
- Human and economic geography by MORGAN, GILLIAN C

iv) ENGLISH LANGUAGE 2

- Bukagire G.R and Nyambari N. (2012) advanced literature, Nyambari Nyangwine publisher Dar es salaam
- Oxford University Press (1992) Oxford Advanced Learner's Dictionary. London: Oxford University Press
- Katatanama, G. (2018). Form six language two review books. Truth Printing Company

v) ENGLISH LANGUAGE 1

- Asheri, N. (2014) Advanced level English: a practical approach 3rd edition Dar es Salaam: Good Books Publishers.
- NORBERT'S ADVANCED LEVEL ENGLISH LANGUAGE – ONE 2rd Edition

vi) GENERAL STUDIES

- Kamili, Z. (2017). General Studies Alive; A straight forward General & Development studies for high school and University students. Dar es Salaam: Kamili Books and General Supplies.

- Mbalase, R.F. (2016) General Studies for advanced level certificate form five. Afrophus industries Ltd.

- Mbalase, R.F. (2016) General Studies for advanced level certificate form six. Afrophus industries Ltd.

4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Katika kipindi cha kusoma hapa shuleni mwanafunzi anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

a) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku
b) Mwanafunzi anatakiwa kuwahi anaposikia wito wa dharura
c) Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa kila mwanzo wa muhula bila kuchelewa
d) Mwanafunzi ni lazima kuhudhuria shule kwa muda wote wa masomo
e) Mwanafunzi ni lazima kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa
f) Mwanafunzi ni lazima kuhudhuria mikutano mbalimbali ya shule
g) Mwanafunzi ni lazima kufanya maandalio kama ilivyopangwa katika ratiba
h) Mwanafunzi ni lazima kufanya kazi zinazotolewa na walimu wa masomo na kukusanya madaftari baada ya maandalio

HESHIMA

a) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
b) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao wenyewe, kwa mwalimu na kwa watu wengine.
c) Ni lazima kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni
d) Ni lazima kuthamini na kuheshimu kazi zote zinazotendeka shuleni

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo awapo shuleni:-

- Mwanafunzi anatakiwa kuitika mara moja na kukimbia alikoitwa.
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali, nembo ya taifa, wimbo wa taifa na fedha za taifa
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia, ofisi ya shule, mali binafsi na mali za uma
- Ni lazima kusimama katika mstari wakati wa kupokea huduma
- Mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mikono juu na asimame anapoulizwa na kujibu maswali.
- Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani asitoke bila ruhusa ya mwalimu

Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuvuta sigara
- Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
- Kugombana
- Kumiliki simu maeneo ya shule
- Kumiliki au kutumia vifaa vya umeme kama vile radio.

SARE ZA SHULE

Ni lazima kila mwanafunzi kuvaa sare wakati wote wa;

- Masomo ya darasani
- Wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
- Mhadhara wa shule
- Anapokwenda hospitali
- Anaposafiri, kuja shuleni au kwenda makwao wakati wa likizo
- Ni lazima sare na mavazi yote yawe safi wakati wote

NB. Kofia au viatu virefu na mapambo mengine yoyote haviruhusiwi kabisa shuleni wala kuchanganywa na sare ya shule.

MIPAKA YA SHULE

i) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule isipokuwa kwa kibali maalumu.

ii) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu :-

- Chumba cha walimu, Ofisi za shule, Maabara, Jikoni, Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.
- Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia sehemu zifuatazo :- Vilabu vya pombe , Majumba ya starehe , Majumba ya kufikia wageni

MALI BINAFSI NA MALI ZA UMMA

Ni kosa kupoteza au kuharibu mali binafsi na za umma.

USAFI

Ni lazima kila mwanafunzi awe msafi mwili na mavazi wakati wote.

UKUMBI WA CHAKULA

- Ni lazima ukumbi wa chakula uwekwe katika hali ya usafi na uheshimiwe.
- Vyakula viliwe ndani ya bwalo tu (hairuhusiwi mwanafunzi kwenda kula kwa Mama lishe).
- Mwanafunzi haruhusiwi kuingia jikoni ila kwa kibali maalum.
- Mwanafunzi afuate taratibu zilizowekwa wakati wa kula chakula.

LUGHA

Ni lazima kuongea lugha ya kiingereza wakati wote mwanafunzi anapokuwa shuleni

5. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa (utoro)
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu ,walezi na jamii kwa ujumla
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote Yule
f) Kufuga ndevu
g) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
h) Uvutaji wa sigara
i) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja au kuoa .
j) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
k) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
l) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
m) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
n) Kudharau Bendera ya Taifa
o) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk
p) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

6. Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule : 

Jina la Mkuu wa Shule : MWASITI B MSOKOLA

Mhuri wa Mkuu wa Shule : 

KIAMBATANISHO "A"



PICHA YA MZAZI/MLEZI

Mimi:……Mzazi/Mlezi.
Ninakubali mtoto wangu……asome katika shule ya Sekondari Kigwe tangu tarehe .....

1. Nimesoma maagizo na kuyaelewa vizuri. Naelewa kuwa Elimu ni haki ya mtoto. Naahidi kutimiza wajibu wangu kwa mtoto. Nitashirikiana na walimu na jamii kwa ujumla kuhakikisha mtoto wangu anakuwa na maadili mema na anapenda kusoma awapo Shuleni na nyumbani pia.

2. Nina ahidi kumpatia vifaa vilivyo tajwa katika orodha.

3. Ninaahidi kuwa nitamhimiza mtoto wangu afanye bidii na kutii sheria zote za shule.

4. Naelewa ya kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia kidato cha tano ni bahati aliyotunukiwa na Taifa. Naahidi ya kuwa nitahakikisha atafuata sheria za shule na ashindwapo hatua zozote zichukuliwe dhidi yake.

…… **…….**
JINA LA MZAZI/MLEZI **SAINI**

Mimi…….. mwanafunzi wa kidato cha tano. Nimesoma na kuzielewa sheria za shule ya Sekondari Kigwe na naahidi kuwa nitazitekeleza kadri ya uwezo wangu.

Sitashiriki katika mgomo wa aina yoyote hapa Shuleni. Nitakuwa mstari wa mbele katika kutunza na kuhifadhi mazingira ya Shule kwa mujibu wa sheria za Shule. Nitatumia juhudi katika kujielimisha na kuhakikisha kwamba wastani wangu kitaaluma ni mzuri.

Nikishindwa kuzitekeleza, hatua zichukuliwe na uongozi wa Shule kulingana na kosa dhidi yangu.

…….. **……**
SAINI YA MWANAFUNZI **TAREHE**

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMNISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

KIGWE SECONDARY SCHOOL.
P.O. Box 656, DODOMA

MEDICAL EXAMINATION FORM:

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Center in respect to all entrants.

Full name:…….Age……..

Sex:…….Year……

1. Blood count
   Red and White):……..…….
2. Urine analysis
   Test……
3. Syphilis Test:……..…….……..…….
4. T.B:……..……..……..…….
5. Ears:…….……..
6. Spleen:…….……..….
7. Abdomen:…….…..

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical impairment, family disease, chronic infections etc.
……
……

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above.

……. **……**
NAME AND DESIGNATION **SIGNATURE AND OFFICAL STAMP**

…… **……**
STATION **DATE**

NOTE:

1. Medical Officer during the Course of this examination please Attend the individual according to any diagnosed case.

2. The dully filled form must be handed to the Head of the School during registration week, Under No circumstances should a student be registered without Certificate of his or her physical fitness.